# Uchambuzi wa Toni kwa Mkabala wa Kiinitoni na Tonijuu Msingi: Uchunguzi wa Lugha ya ki-Meetto -Makuwa cha Tanzania[1]

Joseph Hokororo Ismail

**Ikisiri**

Kumekuwa na taratibu mbalimbali za toni zinazotumika katika uibuzi wa umbo la nje kutoka umbo la ndani. Wataalamu wa fonolojia walioshughulikia toni, mathalani Goldsmith (1976) na Massamba (1982), wamechanganua toni kwa kutumia mkabala uliozingatia matumizi ya kiinitoni ambacho huchombeza utokeaji wa toni; wakati wataalamu wengine kama vile Odden (1989), Batibo (1990), Robert (1992), Matondo (2003) na Marlo (2007) wamechambua toni kwa kutumia mkabala unaozingatia tonijuu msingi kama chanzo cha uibuzi huo. Hawa wa kundi la pili wanaona kwamba kanuni mbalimbali zinazofuatia uibuzi huo huchimbuka kutoka katika tonijuu msingi hiyo. Lengo la makala hii ni kuzungumzia jinsi lugha ya ki-Meetto-Makuwa iliyochanganuliwa kwa misingi ya kiinitoni kuchombeza utokeaji wa toni, inavyoweza kuchambuliwa kwa mkabala unaozingatia tonijuu msingi kama Msingi wa uibuzi. Ingawa mikabala yote ipo katika Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru kama ilivyoasisiwa na Goldsmith (1976), lakini uchambuzi wa toni kwa mkabala wa tonijuu msingi, licha ya kuleta uwazi zaidi, unapunguza pia idadi ya kanuni zinazotumika katika uibuzi huo wa toni na kusaidia kuwa na kanuni chache katika uibuzi wa toni katika ki-Meetto-Makuwa na lugha nyingine za Kibantu.[2]

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inajadili jinsi toni zinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kupachika kiinitoni katika silabi husika na jinsi toni hizi zinavyoweza kuibuliwa kwa kutumia mkabala wa upachikaji tonijuu msingi kama katika silabi maalumu kama chanzo cha uibuzi wa toni katika lugha yenye toni.[3] Mikabala yote miwili ipo katika Kiunzi cha Fonolojia Vipandesauti Huru lakini makala hii inatumia mkabala unaozingatia Tonijuu Msingi (J) kama chanzo cha mchakato wa uibuzi wa toni na hivyo kutumia kanuni chache za toni lakini zenye matokeo bayana ya kiuchanganuzi.

Makala hii inaelezea michakato na kanuni za utokeaji wa toni zinazopatikana katika vitenzi visoukomo vya ki-Meetto-Makuwa. Katika uchanganuzi wa data tumetumia nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru kama ilivyoasisiwa na Goldsmith (1976) na

---

[1] ki-Meetto-Makuwa ni lugha inayozungumzwa kusini mwa Tanzania mpakani mwa Tanzania, na Msumbiji hasahasa katika wilaya za Masasi na Nanyumbu. Kwa mgawanyo wa lugha, Guthrie (1967) aliweka lugha hii katika kanda P kundi 31. Kwa mujibu wa Atlasi ya Lugha za Tanzania (2009), ki-Makuwa kina wazungumzaji 300,825.

[2] Data zilizotumika katika makala hii ni za aina mbili: kwanza kutoka uwandani, kijiji cha Marumba zilikusanywa mwezi Novemba, 2016. Pili, kutoka kazi ya Cheng na Kisseberth (1979).

[3] Kiimbotoni msingi ni ule mzunguko mmoja wa kiimbotoni katika usemaji wa lugha zenye toni (taz. Massamba 2011:173-174 kwa maelezo zaidi).

kutumiwa kwa kiasi kikubwa na wanaisimu mbalimbali kama vile Massamba (1982) Ismail (2011) na Mashauri (2012).

Makala hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inajadili uchambuzi wa toni kwa kutumia mkabala wa awali kabisa wa Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru unaozingatia kiinitoni na sehemu ya pili inajadili uchambuzi wa toni kwa kutumia mkabala unaozingatia tonijuu msingi na kuangalia kama kuna tofauti za msingi baina ya mikabala hiyo. Sehemu ya tatu ni hitimisho la makala.

## 2.0 Uchambuzi wa Toni kwa Mkabala wa Kiinitoni katika ki-Meetto-Makuwa

Katika sehemu hii tunaangalia toni katika vitenzi vya aina mbili ambavyo ni vile visokuwa na yambwa na aina ya pili ni vitenzi visokuwa na ukomo vyenye yambwa.

## 2.1 Toni katika Vitenzi Visoukomo visivyo na Yambwa

Tunaanza mjadala huu kwa kuangalia namna toni katika vitenzi visoukomo visivyo na yambwa inavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia mkabala wa Fonolojia Vipandesauti Huru huku kiinitoni kikiwa msingi wa uibuzi wa toni. Chunguza data ifuatayo (ambapo katika makala hii tonijuu itaoneshwa kwa kuweka alama *[´]* juu ya silabi husika, wakati tonichini haitawekewa alama yoyote):

(1)

| | | |
|---|---|---|
| a. | *up$^h$ítímúla* | kupika ugali mwingi kupitiliza |
| b. | *utátákúla* | kuchubua ngozi, kama ya mti mkavu |
| c. | *ut$^h$árákúla* | kuchambua kama, kama mboga ya majani |
| d. | *ut$^h$órókóla* | kuelezea/kufafanua jambo |
| e. | *usányárára* | kufurahi |
| f. | *ut$^h$úkúrúwa* | kuondoka, kama alfajiri |
| g. | *uhókólósa* | kurejesha |

Katika data 1(a-g) hapo juu tunaona kwamba vitenzi vyote vimeanza na tonichini zikifuatiwa na mkururo wa tonijuu na kumalizikia na tonichini katika silabi ya mwisho. Katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa kiinitoni huhusishwa na toni maalumu miongoni mwa toni zilizopo katika Kiimbotoni Msingi (KTM), yaani Tonichini (C), Tonijuu (J), na Tonichini (C) (Ismail, 2011:45). Aidha, katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa, ili kupata matokeo sahihi katika mchakato wa uibuzi wa toni ni sharti tonijuu ya KTM ihusishwe na silabi ya kwanza ya shina la kitenzi. Hivyo kunapokuwa na mfuatano wa tonijuu katika neno, kinadharia jambo linalotokea ni kwamba tonijuu ya kiinitoni imeisukuma tonichini ya kulia kuelekea kulia mpaka kwenye silabi ya mwisho kasoro moja kutegemeana na urefu wa silabi zilizopo katika kitenzi husika. Hivyo, ili kupata umbo la nje, kanuni zifuatazo za kitoni zinatumika katika uibuzi huo, ambazo ni upachikaji kiinitoni, uhusishaji kiinitoni na KTM, uhusishaji wa KTM na vitamkwa, msambao wa tonijuu kuelekea kulia na Sharti la Ukubalifu. Kwa mujibu wa mkabala huu, alama ya nyota juu ya silabi husika inamaanisha silabi hiyo ndiyo iliyobeba kiinitoni msingi (CJC) katika lugha inayochanganuliwa.

Tukifuata kanuni hizi kwa jinsi ya utokeaji wake, neno kama *[usányárára]* *'kufurahi'* huchanganuliwa kama ifuatavyo:

(2) *u sá nyá rá ra* kufurahi

*
*u sa nya ra ra* Upachikaji kiinitoni

*
*u sa nya ra ra*
CJC Uhusishaji kiinitoni na KTM

*
*u sa nya ra ra*
C J C Uhusishaji KTM na vitamkwa

*
*u sa nyara ra*
C J C Usambaaji kulia Tonijuu

*u sa nya ra ra*
C J J J C *[u sá nyá rá ra]*


Kama tunavyoona katika uibuzi huo hapo juu, kanuni hizi hutupatia matokeo sahihi ya toni katika ki-Meetto-Makuwa. Tuchanganue mfano mmoja zaidi katika (3) hapa chini:

(3*)* *u rú kú nú sa* kugeuza

*
*u ru ku nu sa* Upachikaji Kiinitoni

*
*u ru ku nu sa*
CJC Uhusishaji Kiinitoni na KTM

*
*u ru ku nu sa*
C J C Uhusishaji KTM na Vitamkwa




Usambaaji Kulia Tonijuu

*[ u rú kú nú sa]*

Tukichunguza data (3) tunaona kwamba uchambuzi wake umehusisha maneno yenye ukomo wa silabi nne. Lakini tunapoabiri data yenye silabi nne au zaidi, muundo wa toni zake hubadilika kama inavyoonekana katika (4):

| | | | |
|---|---|---|---|
| (4) | (a) | *up^hírίkitúwa* | kuvingirika |
| | (b) | *uwúrúwurúwa* | kuzunguka |

Tukiangalia mifano katika (4) hapo juu tunaona kwamba tabia ya utokeaji wa toni ni tofauti kabisa na jinsi toni zilivyojitokeza katika (1). Katika (4) hapo juu tunaona kwamba, tonijuu husambaa kuelekea kulia mpaka kwenye silabi ya pili ya shina. Muundo wa toni zake unaanza kwa utokeaji wa tonichini ikifuatiwa na mfululizo wa tonijuu ikifuatiwa na tonichini na silabi ya mwisho kuwa ya tonijuu.Swali la msingi la kujiuliza hapa ni kwa vipi utokeaji wa tonichini katika silabi ya tatu kutoka mwisho inaweza kufafanuliwa?Ufafanuzi wa swali hili ni wa kinadharia zaidi kwamba vitenzi visoukomo vyenye silabi zaidi ya nne vinakuwa na KTM viwili, KTM cha kwanza ni katika silabi ya kwanza ya shina na KTM kingine ni katika silabi ya mwisho kasoro moja. Utokeaji wa KTM ya pili unaweza kuelezeka kinadharia kwamba KTM ya kwanza ndicho kinachonakiliwa katika silabi hiyo ya mwisho kasoro moja na hivyo kuwa na kanuni ya unakiliji wa KTM. Hivyo, tunatengeneza sheria ya toni kubainisha utokeaji wa KTM katika kitenzi kisoukomo kama ifuatavyo (katika makala hii * huonesha kiinitoni,** huonesha umbo kutokuwa sahihi kisarufi, *$* sehemu, # mwanzo au mwisho wa neno na *KI* silabi yenye konsonsnti na irabu:

**Kanuni 1: Unakiliji wa Kiinitoni Shina**

*- - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - ►*


# + KI KI ………………… KIKI KI#

Kit

Kanuni hii inasema kwamba kiinitoni katika silabi ya kwanza ya kitenzi hunakiliwa katika silabi ya mwisho kasoro moja.


Kwa kutumia kanuni hii, tunaweza sasa kuchanganua vitenzi visoukomo vilivyomo katika (4) kwa kutumia mifano miwili *ya* *[up$^h$íríkitúwa]* na *[up$^h$irikituwela]* katika (5) na (6) hapa chini:

(5) *up$^h$íríkitúwa* ‘kuvingirika’




Hapa tunapata matokeo yanayokubalika katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa. Tukiongeza silabi ya tano katika umbo la utendea, uibuzi wa toni kwa kitenzi kisoukomo kama */up$^h$íríkítuwéla/* inakuwa kama ifuatavyo:

(6)




Hapa pia tunapata matokeo kubalifu katika lugha hii.

Tumalizie uchambuzi wa vitenzi visoukomo kwa kuangalia vitenzi visoukomo vyenye silabi mbili. Tofauti kubwa ya kundi hili na vile tulivyokwishavitazama inahusu tabia ya toni zake. Muundo wa toni katika kundi hili hauna usambaaji wa tonijuu. Tutazame mifano katika data ifuatayo:

(7)

a) *up$^{h}$éla* kuchoka
b) *up$^{h}$ícha* kuchelewa
c) *ut$^{h}$ípa* kuchimba
d) *ut$^{h}$íta* kutwanga
e) *ut$^{h}$úma* kununua

Katika (7) tunaona kwamba muundo wa toni huanza na tonichini, ikifuatiwa na tonijuu katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi na mwisho tonichini katika silabi ya mwisho. Katika muundo huu wa toni pia hakuna msambao kulia wa tonijuu. Kinadharia, sababu ya kutokuwa na usambaaji wa tonijuu ni kwamba tonijuu ya KTM haiwezi kuisukuma tonichini ya kulia kwa sababu iko katika silabi ya mwisho ya neno. Hivyo, kanuni za toni zinazohusika katika uchambuzi wake ni kama inavyoonekana katika (8) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| (8) | *u ví t$^{h}$a* | kuficha |
| | * | |
| | *u vi t$^{h}$a* | Upachikaji Kiinitoni |
| | * | |
| | *u vi t$^{h}$a* | |
| | \| | |
| | CJC | Uhusishaji Kiinitoni na KTM |
| | * | |
| | *u vi t$^{h}$a* | |
| | \| \| \| | |
| | C J C | Uhusishaji KTM na Vitamkwa |
| | *u vi t$^{h}$ a* | |
| | \| \| \| | |
| | C J C | *[uvít$^{h}$a]* |

Hapa pia tunapata matokeo kubalifu kitoni.

Hivyo, kama inavyojitokeza katika uibuzi huu, hakuna tabia ya msambao wa tonijuu na kwamba kanuni chache tu za uibuzi ndizo zinazotumika tofauti na vitenzi vile visoukomo vyenye silabi zaidi ya tatu. Katika sehemu inayofuata tunaangalia kwa kifupi tabia ya toni katika vitenzi visoukomo vyenye yambwa.

## 2.2 Toni katika Vitenzi visoukomo vyenye Yambwa

Lugha ya ki-Meetto-Makuwa inaruhusu kuwa na kitenzi kisoukomo chenye yambwa moja tu ambayo hujitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi. Kuwapo kwa yambwa hiyo huathiri tabia yote ya toni katika ki-Meetto-Makuwa kwa kuwa mofimu ya yambwa inakuwa na Kiinitoni ambacho huchombeza utokeaji tonijuu. Tuangalie mifano katika data ifuatayo (9):

(9)

| | | |
|---|---|---|
| a) | *umútótókóléla* | kumchania, kama karatasi |
| b) | *umúhókólóséa* | kumrudishia |
| c) | *umúvénékúléla* | kumgeuzia (kama macho) |
| d) | *umúvíchíkánéla* | kumjazilizia |
| e) | *umúwílíphíléa* | kumlindia kwa bidii |
| f) | *umúwónyókóléla* | kumnolea makali (kama panga) |

Maumbo ya yambwa (yaliyopigiwa mstari, ambayo ni nafsi ya kwanza umoja) huambikwa kabla ya mashina ya vitenzi husika. Tunaona pia, kwa mfano, kwamba vitenzi vyote vyenye yambwa huwa na msambao wa tonijuu. Hivyo kitenzi kinaanza na tonichini, ikifuatiwa na mfululizo wa tonijuu iliyosambaa kuelekea kulia mpaka kwenye silabi ya mwisho kasoro moja ambayo inakuwa na tonichini. Kutokana na hali hii, inaweza kudhaniwa na mchambuzi kwamba kwa kuwa tonijuu hujitokeza mara tu baada ya kiambishi awali cha kitenzi */u-/* isoukomo, na kufuatiwa na tonijuu ya umbo la yambwa basi tonijuu hii ya yambwa ndiyo inayosambaa kuelekea kulia kabla ya kanuni nyingine za toni; jambo ambalo si sahihi kwa mujibu wa uchambuzi wa kutumia mkabala wa fonolojia ya vipandesauti Huru.

Kinadharia, maumbo ya ndani ya vitenzi visoukomo vyote vyenye yambwa katika ki-Meetto-Makuwa huwa yanakuwa na viinitoni viwili: kiinitoni cha kwanza kinakuwa katika silabi ya kwanza ya shina la kitenzi na kiinitoni cha pili kinakuwa katika mofimu ya yambwa. Tunapoangalia mchakato wa ujitokezaji wa toni katika umbo la nje la neno kutoka umbo la ndani kwa kutumia viinitoni hivi viwili tunapata matokeo yafuatayo:

(10) *u mú ká vé la* — kumchunia (kama ngozi)

* *
*u mu kave la* — Upachikaji Kiinitoni

* *
*u mu ka vel a*

CJCCJC — Uhusishaji Kiinitoni na KTM

* *
*u mu ka ve la*


C J CC J C — Uhusishaji KTM na Vitamkwa

* *
*u mu ka ve la*

C J C CJ C C — *[** umûkăvela]*

Ujitokezaji wa toni katika umbo la nje linalopatikana linatofautiana na umbo la ki-Meetto-Makuwa linalokubalika. Katika mfano huo tunapata umbo lisilokubalika kikanuni, yaani [** *um ûkăvela]*. Kinadharia na kwa kutumia mkabala wa fonolojia ya vipandesauti huru, umbo la nje limepatikana baada ya kuendelea kuvitumia viinitoni vyote viwili katika mchakato wa ukokotoaji wa umbo la nje. Vitenzi visoukomo vyenye yambwa vinapokuwa na viinitoni viwili katika mkururo mmoja, kikanuni katika lugha hii, kinitoni cha silabi ya kwanza ya shina hudondoka na kubaki na kiinitoni cha silabi ya yambwa. Hii ni kwa sababu kiinitoni cha silabi ya kwanza ya shina na ina hadhi ya chini kuliko kiinitoni katika yambwa. Kiinitoni cha silabi ya kwanza ambacho ndicho chenye hadhi ya chini hudondoka kwa kutumia kanuni ya udondoshaji wa kiinitoni cha shina, ambayo ni kanuni mojawapo ya toni katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa (Ismail, 2011: 95). Tunairejea kanuni hii hapa chini kama ifuatavyo:

**Kanuni 2: Udondoshaji Kiinitoni Shina**




Katika kanuni hii, kiinitoni katika silabi ya kwanza ya shina hudondoka kinapotanguliwa na kiinitoni cha silabi ya yambwa. Baada ya kudondoka kwa kiinitoni cha silabi ya shina, tunabaki na kinitoni cha yambwa ambacho sasa hutengeneza mazingira kwa kanuni nyingine za toni kama vile msambao kulia wa tonijuu kujitokeza. Hivyo kanuni ya ukokotoaji wa maumbo ya nje kutoka maumbo ya ndani katika vitenzi visoukomo vyenye yambwa huhusika na tonijuu ya kiinitoni kusukuma tonichini kuelekea kulia mpaka silabi ya mwisho kasoro moja, kama katika mfano wa neno *[umúvít$^h$éla]* 'kumfichia' unavyochanganuliwa hapa chini katika (11):


(11) *u mú ví t$^h$é la* kumfichia

*    *
*u mu vi t$^h$e la* Upachikaji Kiinitoni


*  (*)
*u mu vi t$^h$ela* Udondoshaji Kiinitoni Shina

*
*u muvi t$^h$ela*


|
CJC Uhusishaji Kiinitoni na KTM




Uhusishaji wa KTM na Vitamkwa




Usambaaji Kulia Tonijuu




*[umúvítʰéla]*

Hapa tunapata kitenzi chenye ujitokezaji wa toni unaokubalika katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa. Baada ya mifano hiyo, sasa tuangalie jinsi uchanganuzi wa toni katika maneno yenye silabi tano au zaidi zikiwa na yambwa. Tazama mifano ifuatayo:

(12)

| | | |
|---|---|---|
| a) | *umúwúnúkuléla* | kumfunulia |
| b) | *umúsányáraréla* | kumfurahia |
| c) | *umúsháshámuréla* | kumchashusha, hasa pombe |
| d) | *umúshóróroweéla* | kumchovyea, hasa kimiminika |
| e) | *umúyúkúvaléla* | kumwivishia, kama ndizi sio kwa kupika |
| f) | *umúnyópócholéla* | kumnyongea (shingo) |

Katika data (12) hapo juu tunaona kwamba silabi ya mwisho kasoro mbili katika vitenzi visoukomo vyenye silabi tano au zaidi huku vikiwa na yambwa, inakuwa na tonichini ikifuatiwa na tonijuu na kisha tena neno kuishia na tonichini. Katika vitenzi visoukomo vyenye mfuatano wa toni kama huu, kunakuwa na viinitoni viwili, kiinitoni cha kwanza ni lile kilichopo katika silabi ya kwanza ya shina na kiinitoni cha pili ni kile cha yambwa. Hivyo ili kupata kitenzi kinayokubalika katika ki-Meetto-Makuwa, kwa vitenzi visoukomo vyenye yambwa, kunakuwa na kanuni ya uhamishaji wa kiinitoni shina kwenda katika silabi ya mwisho kasoro moja. Kanuni hii inaweza kuandikwa kama ifuatavyo hapa chini (3):

**Kanuni 3: Uhamaji Kiinitoni Shina**


*- - - - - - - - - -►*

*#u$KI $ KI $ KI $ KI$ KI$ KI$ #*

shina

Kanuni hii inasema kwamba, kiinitoni cha silabi ya shina huhamia katika silabi ya mwisho kasoro moja. Hivyo kwa kutumia kanuni hii (3), ukokotoaji wa toni kwa vitenzi visoukomo vyenye yambwa kwa data (12), unakuwa kama ifuatavyo hapa chini:

(13) *u mú tʰá r áku lé la* kumchambulia (kama mboga za majani)




Upachikaji Kiinitoni

Uhamaji Kiinitoni shina

Uhusishaji Kiinitoni na KTM

Uhusishaji KTM na Vitamkwa

Usambaaji Kulia Tonijuu

Udondoshaji Tonichini

*[umútʰárákuléla]*

Ukokotozi huu unatupa neno linalokubalika katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa.

Baada ya kuangalia namna ambavyo kiunzi cha Fonolojia Vipandesauti kinavyofanya kazi kwa kutumia mkabala wa kiinitoni, yapo maswali ya msingi ya kinadharia

tunayopaswa kujielekeza. Kwanza, ni kuhusu uwingi wa kanuni zinazotumika na changamoto ya matumizi ya nyota katika kuwakilisha kiinitoni kinachochombeza tonijuu. Pili, matumizi ya kiimbotoni msingi kama vile CJC kuelekezwa katika silabi moja iliyowakilishwa na alama ya nyota (*). Masuala haya tunayajadili hapa chini kwa kuabiri misingi ya mkabala wa tonijuu na jinsi unavyofanya kazi huku tukitumia data zenye muundo unaofanana na tulioutumia hapo juu. Baada ya hapo tutaona ufaafu wa mkabala huu kulinganisha na mkabala tuliouangalia hapo juu. Jambo la msingi la kuelewa hapa ni kwamba pamoja na tofauti ya mikabala hii, mikabala yote miwili ipo katika kiunzi cha Fonolojia Vipandesauti huru na masuala yanayojitokeza na tofauti zake ni maboresho tu katika maendeleo ya kiunzi hiki.

## 3.0 Uchambuzi wa Toni kwa Kutumia Mkabala wa Tonijuu Msingi katika ki-Meetto-Makuwa

Wataalamu mbalimbali katika taaluma ya toni kama vile Batibo (1990), Marlo (2007), Odden (1989), kuwataja wachache, waliboresha kiunzi cha Fonolojia Vipandesauti Huru, kwa kuanza kuzichambua toni za lugha kwa mtazamo wa tonijuu kama msingi wa ujitokezaji wa toni katika umbo la nje badala ya kutumia mkabala wa toni kuchombezwa na kiinitoni. Mkabala wa Tonijuu Msingi hutumia Tonijuu (J), kama msingi wa ukokotozi. Tonijuu hii (J) huwekwa juu au chini ya silabi husika kama inavyoonyeshwa katika ukokotozi hapa chini.

### 3.1 Toni katika Vitenzi Visoukomo visivyo na Yambwa

Kimsingi jambo linalotofautisha uchambuzi wa toni kwa kutumia kiinitoni msingi na ule mkabala wa Tonijuu Msingi ni idadi ya sheria za ukokotozi. Katika mkabala unaotumia Tonijuu Msingi, toni chini hupachikwa kwenye hatua ya mwisho kwa kanuni ya uhusishaji wa vitamkwa na toni chini. Hivyo ili kupata umbo la nje, kwa kutumia mkabala huu, kanuni zinazotumika ni upachikaji Tonijuu Msingi, usambaaji kulia Tonijuu, uhusishaji kitamkwa na tonichini na kadhalika kutegemeana na aina ya kitenzi husika. Kumbuka tumesema kwamba ili kupata umbo linalokubalika katika ki-Meetto-Makuwa, kuna kanuni ya Uhusishaji toni chini na kitamkwa chochote kisichohusishwa na toni yoyote. Hivyo tunaichonga kanuni ya uhusishaji tonichini na irabu kama ifuatavyo hapa:

**Kanuni 4**: Uhusishaji Tonichini na Irabu

$$\emptyset \longrightarrow \begin{array}{c} C \\ | \\ I \end{array}$$

Hivyo ukokotozi wa vitenzi katika kundi hili kama *[usányárara]* 'kufurahi' *na [u rú kú nú sa]* 'kugeuza' inakuwa kama ifuatavyo:

(14) u sá nyá rá ra kufurahi

u sa nya ra ra — Upachikaji Tonijuu
J
u sa nyara ra
J — Usambaaji Kulia Tonijuu
u sa nyara ra
C J C — Uhusishaji Vitamkwa na Tonichini
u sanya rara
C J J J C — [usányárára]

Kama tunavyoona katika ukokotozi huo hapo juu, kanuni hizi hutupatia matokeo sahihi ya toni katika ki-Meetto-Makuwa. Tuchanganue mfano mmoja zaidi katika (15) hapa chini: */u rú kú nú sa/* ‘kugeuza’.

**(**15**)**

*u ru ku nu sa* — Upachikaji Tonijuu
J
*u ruku nu sa*
J — Usambaaji Kulia Tonijuu
*u rukunu sa*
C J C — Uhusishaji Vitamkwa na Tonichini
*u ru ku nu sa*
C J J J C — *[urúkúnúsa]*

Tukichunguza data (14) na (15) tunaona kwamba uchambuzi wake umehusisha maneno yenye ukomo wa silabi nne. Lakini tunapoabiri vitenzi visoukomo vyenye silabi nne au zaidi, muundo wa toni zake hubadilika. Tuangalie data ifuatayo:

(16)

a) *upátákuléla* — kufunulia
b) *urúkúnuléla* — kugeuzia

c) *upárángandéla* kupangilia
d) *upútúkuréla* kufunikia

Tukiangalia data katika (16) hapo juu, tunaona kwamba tabia ya utokeaji wa toni kwa kutumia mkabala wa upachikaji Tonijuu Msingi ni tofauti kabisa na jinsi toni zilivyojitokeza katika (1). Katika mifano hii tunaona kwamba msambao wa tonijuu huelekea kulia na kukoma katika silabi ya mwisho kasoro mbili. Muundo wa toni zake unaanzia na tonichini ikifuatiwa na mfululizo wa tonijuu ikifuatiwa na tonichini na silabi ya mwisho kasoro moja huwa na tonijuu na kumalizikia na tonichini. Swali la msingi la kujiuliza hapa ni kuhusu utokeaji wa tonichini katika silabi ya mwisho kasoro mbili. Ufafanuzi wa swali hili ni wa kinadharia zaidi kwamba vitenzi visoukomo vyenye silabi zaidi ya nne vinakuwa na Tonijuu Msingi mbili. Tonijuu Msingi ya kwanza inapachikwa katika silabi ya kwanza ya mzizi na Tonijuu Msingi ya pili inakuwa katika silabi ya mwisho kasoro moja katika kitenzi husika. Utokeaji wa Tonijuu Msingi ya pili unaweza kuelezeka kinadharia kwamba Tonijuu Msingi ya shina ndiyo inayonakiliwa kwenye silabi hiyo ya mwisho kasoro moja. Hivyo tunatengeneza kanuni ya toni kubainisha utokeaji wa Tonijuu Msingii katika kitenzi kisoukomo cha mwisho kasoro moja kama ifuatavyo:

**Kanuni 5: Unakiliji Tonijuu**


**J ⟶ J**
I *$* KI *$* KI *$* *KI* *$* KI *$* #
shina

Kanuni hii inaeleza kwamba Tonijuu katika silabi ya kwanza ya kitenzi hunakiliwa katika silabi ya mwisho kasoro moja.


Kwa kutumia kanuni hii, tunaweza kuchanganua tena vitenzi visoukomo vilivyomo katika (4) kwa kutumia mifano miwili ya /*u$p^h$íríkitúwa*/ na */u $p^h$i ríkituwéla*/ katika (17) na (18) hapa chini:

(17) u $p^h$i rí ki tú wa kuvingirika

J
u $p^h$i ri ki tu wa Upachikaji Tonijuu
J ⟶ J
u $p^h$i ri ki tu wa Unakiliji Tonijuu



Usambaaji Kulia Tonijuu



Usahisishaji Tonijuu

u p$^{h}$i ri ki tu wa

C J J C J C — Uhusishaji vitamkwa na tonichini

u p$^{h}$i ri ki tu wa

C J J C J C — *[u p$^{h}$í rí ki tú wa]*

Kanuni zilizotumika kuibua toni katika (17), zinaweza kutumika pia kuibua toni katika kitenzi kisoukomo /*up$^{h}$írikituwéla/, kama* inavyoonekana hapa chini (18):

(18) *u p$^{h}$i ri ki tu wé la* — kuvingirikia

J
*u p$^{h}$i ri ki tu we la* — Upachikaji Tonijuu

J → J
*u p$^{h}$i ri ki tu we la* — Unakiliji Tonijuu

*u p$^{h}$i ri ki tuwela*

J J — Usambaaji Kulia Tonijuu

*u p$^{h}$i ri ki tuwela*

J J — Urahisishaji Tonijuu

*u p$^{h}$i ri ki tu we la*

C J J J C J C — Uhusishaji Tonichini na vitamkwa

*u p$^{h}$i ri ki tu we la*

C J J J C J C — *[u p$^{h}$í rí kí tu wé la]*

Hapa pia tunapata matokeo kubalifu katika lugha hii.

Tumalizie uchambuzi wa toni kwa kuangalia vitenzi visoukomo vyenye silabi mbili. Tutatumia data katika 7 hapo juu katika uchambuzi wa toni katika kundi hili la vitenzi. Muundo wa toni katika kundi hili unakuwa na tonichini kukifuatiwa na tonijuu na kumalizikia tonichini. Hivyo kwa kutumia kanuni za Upachikaji tonijuu Msingi na Uhusishaji tonichini na Vitamkwa, uchambuzi wake unakuwa kama ifuatavyo:

(19) *u ví $t^h$a* kuficha

J
*u vi $t^h$a* Upachikaji Tonijuu

*u vi $t^h$a*
| | |
C J C Uhusishaji Vitamkwa na Tonichini

*u vi$t^h$ a*
| | |
C J C *[uví$t^h$a]*

Hapa pia tunapata matokeo kubalifu katika lugha hii kuhusiana na toni

## 3.2 Toni katika Vitenzi Visoukomo vyenye Yambwa

Maumbo haya tulikwishayajadili katika sehemu ya kwanza ya makala hii (tazama data 12), hivyo katika sehemu hii tutajielekeza moja kwa moja katika uchanganuzi wa vitenzi hivi kwa kutumia mkabala wa Tonijuu Msingi kama chanzo cha mifanyiko ya kitoni na kuangalia tofauti za msingi za kikanuni kati ya mkabala huu na ule wa awali wa matumizi ya kiinitoni kama msingi wa uchombezaji toni. Mifano;

(20) u mú ká vé la kumchunia (ngozi)

J J
u mu ka ve la Upachikaji Tonijuu

u mu ka ve la
| |
u mu ka ve la
| |/
J J Usambaaji Kulia Tonijuu

umu ka ve la

C J J C Uhusishaji vitamkwa na Tonichini

umu ka ve la

C J J J C *[ umúkávéla]*

Hapa tunaona bayana kwamba, kwa kutumia njia hii, tunapata kitenzi kinachoonekana *kukubalika* kitoni katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa. Tatizo la kutumia njia hii ni la kinadharia. Hakuna maelezo ya kinadharia kuhusu hadhi ya Tonijuu Msingi iliyopo katika umbo la yambwa */mú/* kwa sababu tonijuu inayoonekana hapa ni ile ya Tonijuu Msingi.

Njia nyingine ambayo mwanafonolojia anaweza kushawishika kuitumia katika kuibua toni zilizomo katika kitenzi hicho ni kufikiri kwamba, kitenzi hiki kina Tonijuu Msingi moja katika silabi ya kwanza ya shina na kwamba Tonijuu hii ndiyo iliyohama / kuruka nyuma mpaka kwenyekiambishi cha yambwa *[mú]*. Kutokana na kuhama huku, kunakuwa na umuhimu wa kutengeneza kanuni itakayohusika na uhamaji huo kama inavyopendekezwa hapa chini:

**Kanuni 6: Mrukonyuma wa Tonijuu Msingi**

**J ⟵ J**

I $ KI $ KI $ KI $ KI $ #

yambwa shina

Kanuni hii inasema kwamba tonijuu Msingi ya kiambishi cha shina imeruka silabi moja nyuma mpaka kwenye kiambishi cha yambwa.

Hivyo uchanganuzi wa toni kwa kutumia kanuni hii inakuwa kama ifuatavyo:

(21)

J

u mu ka ve la Upachikaji Tonijuu


u mu ka v el a

⟵

J Mrukonyuma Tonijuu

u mu ka ve la

J





Usambaaji Kulia Tonijuu

Uhusishaji Vitamkwa na Tonichini

*[umúkávéla]*

Matumizi ya kanuni katika (21) hutuonesha kwamba, kwa kufuata mpangilio huo wa kanuni za uibuzi tumepata matokeo yanayokubalika kitoni/ kimatamshi katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa, lakini kinadharia sio sahihi. Maelezo ya kinadharia yanayoweza kutupatia maumbo yanayokubalika kitoni ni kwamba katika vitenzi visoukomo vyenye kiambishi yambwa, kuna Tonijuu Msingi mbili. Tonijuu Msingi ya kwanza, kama kawaida ya mahitaji ya lugha hii, ipo katika silabi ya kwanza ya shina na Tonijuu Msingi ya pili ipo katika kiambishi cha yambwa. Iwapo Tonijuu Msingi hizi mbili zikiachwa ziendelee kubaki katika mchakato wa uibuzi, tunapata tatizo la kinadharia hasa katika sentensi ndefu zenye toni msambao kama zile zinazohitaji urahisishaji wa tonijuu. Hivyo, kama tulivyojadili hapo juu, katika mazingira ambayo vitenzi visoukomo vyenye yambwa vinapokuwa na tonijuu msingi mbili, toni juu ya silabi ya kwanza ya kitenzi hicho hudondoka/ hurahisishwa. Kudondoka huku hutengeneza mazingira ya kubaki tonijuu msingi katika silabi ya yambwa pekee na hapo ndipo huwa chanzo cha mifanyiko ya uibuzi wa toni kama vile msambao kulia wa tonijuu. Hivyo, ili kupata umbo linalokubalika kitoni tutarejea kanuni (2) urahisishaji wa kiintoni ambayo tutaiita kuwa ni kanuni ya Urahisishaji Tonijuu Msingi. Kanuni hii itatumika pale tu tonijuu msingi ya kitenzi kisoukomo changamani kitakapotanguliwa na tonijuu msingi ya kiambishi cha yambwa. Kanuni inayopendekezwa hapa ni hii ifuatayo katika (7):


**Kanuni 7: Urahisishaji Tonijuu Msingi ya Shina**




Kanuni hii husema kwamba tonijuu msingi katika shina hudondoka inapotanguliwa na tonijuu msingi yenye kiambishi yambwa.


Hivyo kwa kutumia kanuni ya urahisishaji Tonijuu Msingi (7) na msambao kulia wa tonijuu, data katika (12) zinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo hapa chini: *[umúvít$^{h}$éla ]* ‘kumfichia’, kama ifuatavyo:


(22)





Tuangalie pia (23) hapa chini jinsi ukokotoaji wa toni katika kitenzi kisoukomo chenye zaidi ya silabi tano:

(23)







Urahisishaji Tonijuu




Uhusishaji Vitamkwa na Tonichini




*[umút$^{h}$árákuléla]*

Je, kuna tofauti gani ya msingi inayojionesha kati ya uibuzi kwa kutumia Tonijuu Msingi na ule tuliouona katika (2.0) unaochombezwa na kiinitoni? Tofauti za msingi zinazojitokeza katika uchanganuzi unaotumia kiinitoni na ule unaotumia tonijuu kama misingi ya ujitokezaji wa toni katika maumbo ya nje ya maneno ya lugha hii ni kwamba; kimsingi hakuna tofauti katika utumiaji wa mikabala yote miwili kwa sababu yote ina usambaaji tonijuu, urahisishaji wa toni, udondoshaji, uhusishaji wa ama tonijuu au kiinitoni, nk. Tofauti ipo katika kuhusisha kiimbotoni msingi ambapo katika mkabala wa tonijuu msingi kumetumika 'uhusishaji wa tonichini'. Kwa hiyo, hatua ni zilezile na idadi ya kanuni ni zile zile.

Pamoja na tofauti hizo, bado zote zinatumia kanuni na kwamba njia ya kupunguza zaidi matumizi ya kanuni za uibuzi inafaa kuchukuliwa. Aidha, Makala hii inaonesha kwamba lugha ambazo toni zake zimechanganuliwa kwa njia ya mkabala unaozingatia kiinitoni zinaweza kuchanganuliwa pia kwa kutumia mkabala wa Tonijuu Msingi na bado ikaleta matokeo yanayokubalika katika lugha ya ki-Meetto-Makuwa na lugha nyingine za Kibantu.

## 4.0 Hitimisho

Katika makala hii tumejadili tabia ya toni katika ki-Meetto-Makuwa kwa kutumia Nadharia ya Phonolojia Vipandesauti Huru. Makala imelinganisha namna toni zinavyoweza kushughulikiwa kwa kutumia mkabala wa kutumia kiinitoni kama kitu muhimu kinachochombeza utokeaji wa toni na mkabala wa Tonijuu Msingi. Makala

imeonesha kwamba kwa kutumia mikabala yote miwili bado matokeo yanayopatikana kutokana na uibuzi wa toni yanafanana. Kwamba, ili kupata maumbo ya nje kutoka maumbo ya ndani zipo kanuni za msingi za kitoni kama vile upachikaji wa kiinitoni au upachikaji Tonijuu Msingi, urahisishaji na udondoshaji wa kiinitoni msingi cha shina au tonijuu ya shina, usambaaji kulia wa Tonijuu na uhusishaji wa vitamkwa na tonichini.

Tumeona pia kwamba katika vitenzi visoukomo vyenye kiambishi yambwa kunakuwa na Tonijuu Msingi mbili au viinitoni viwili na hivyo baada ya kanuni ya Urahisishaji Tonijuu Msingi au kiinitoni katika silabi ya kwanza ya shina, Tonijuu Msingi ya Yambwa au kiinitoni cha yambwa hunakiliwa katika silabi ya mwisho kasoro moja na hivyo michakato mingine ya uibuzi huendelea kufanyika. Mjadala umeonesha kwamba ingawa mikabala yote miwili hutupatia matokeo kubalifu yanayofanana lakini njia zote hizi zina mzunguko kikanuni. Michakato inatumia nadharia nyingi zinazokosa uwekevu.

**Shukurani:**
Ninamshukuru Profesa Massamba kwa kunifundisha fonolojia mpaka ninaweza kujieleza vizuri ipasavyo katika uwanja huu. Vilevile, ninamshukuru Professa Kahigi kwa kusoma kazi hii na kunipatia maoni kadhaa. Bila kuwasahau wahariri wa *Kioo cha Lugha* kwa kukubali kuchapisha makala hii. Pia, ninawashukuru wanafunzi wangu wa Umahiri katika Isimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaamu 2015/2016 na Chuo Kikuu cha Mt. Agustino Mwanza kwa jinsi wanavyonipa maoni na changamoto mbalimbali zinazohusu toni katika lugha zao hasa zile za Kibantu. Hata hivyo, udhaifu wowote katika kazi hii hauwahusishi hawa niliowashukuru.

## Marejeleo

Batibo, H. M. (1990). The Two-directional Tone Melody Spread in Sukuma, Berkeley, *Linguistic Society*. 17:15-24.

Cheng, C. C. & C. W. Kisseberth. (1979). “Ikorovere Makua Tonology (part I)” in *Studies in the Linguistic sciences* 9.1: kur.31-64.

Goldsmith, J. (1990). “Prosodic Trends in the Bantu Languages” In Smith, N and H.Hulst, (wah.), in *Autosegmental Studies in Pitch Accent*. kur.121-144. Dordrecht: Foris Publications.

Goldsmith, J. (1976). “An overview of Autosegmental Phonology”, Indiana University Linguistics Club, Bloomington.

Guthrie, M. (1967). Comparative Bantu, juzuu. 1. Farnborough: Gregg.

Ismail, J.H. (2011). “A Tonological Study of Meetto-Makuwa of Southern Tanzania”. Unpublished Ph.D dissertation, University of Dar es Salaam.

Marlo, M. (2007). “The verbal tonology of Lunyala and Lumarachi: Two Dialects of Luyia.” PhD. Dissertation, University of Michigan.

Mashauri, M. A. (2012). “Toni katika Nomino za Lugha ya ki-Konongo.” Tasinifu ya MA. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (1982). “Aspects of Accent and Tone in Ci-Ruri”. Unpublished Ph.D dissertation. Indiana University.

Massamba, D. P. B. (2010). *Phonological Theory: History and Development*. DSM: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). Maendeleo katika Nadharia ya Phonolojia. Dar es Salaam: TATAKI

Matondo, M. (2003). Tonal and Prosodic Morphology in Kisukuma, Ph.D Dissertation, UCLA.
Mradi wa Lugha za Tanzania. (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania.* Dar es Salaam.
Odden, D. (1989). Predictable tone systems in Bantu. In H. Smith van de Fulst and N. (wah.) Autosegmental studies on pitch accent system, kur. 225-251. Dordrecht: Foris.
Robert, R.R. (1992). Anon-metrical Theory of Sukuma tone. Ohio State University Working Papers in Linguistics 41.135-148.